



**Taarifa za Mzazi kuhusu Elimu ya Maisha ya Familia
Gredi ya 4 - 5**

“Viwango vya Virginia vya elimu ya maisha ya familia hutoa mtaala wa kina na wa mfululizo wa Chekechea hadi Gredi ya 12. Inajumuisha mafunzo yanayoambatana na umri kuhusu maisha ya familia na mahusiano ya jamii, elimu ya kujiepusha na ngono, umuhimu wa kusubiri kabla ya kujihusisha na vitendo vya ngono, maumbile ya kingono na elimu ya uzazi wa binadamu. Mafunzo yamesanifiwa hivi kwamba yanahimiza uhusikaji wa wazazi, kuchochea dhana bora za kibinafsi na kutoa mbinu za kukabiliana na shinikizo la wanarika na changamoto za maisha ya kisasa kulingana na hatua za ukuaji na uwezo wa wanafunzi.” (<https://www.doe.virginia.gov/teaching-learning-assessment/instruction/family-life-education>)

Nyenzo zote za mafunzo zinazotumika kwenye elimu ya maisha ya familia zimeidhinishwa na kukaguliwa na Kamati ya Ushauri wa Afya ya Shuleni ya Hampton City Schools. Wazazi na walezi wana haki ya kukagua mpango wa Elimu ya Maisha ya Familia unaotolewa na kitengo cha shule yao, ikiwa ni pamoja na nyenzo zote zilizoandikwa na za ziada zinazotumika kwenye mpango huo.

Njia za kukagua nyenzo:

- Unaweza kupata muhtasari wa mada na masomo kwenye [tovuti](#) ya Elimu ya Afya na Siha, kwenye kichupo cha Elimu ya Maisha ya Familia.
- Wazazi wanaweza kuangalia nyenzo za mafunzo mtandaoni kupitia **Parent Square** kwa kuingia katika akaunti na kubofya Kiungo cha Nyenzo.
- Nakala halisi ya nyenzo zote zilizochapishwa na maelezo ya nyenzo zote za sauti na video huwekwa kwenye kituo cha maudhui cha shule au kwenye matunzio ya ofisi kuu na hutolewa kwa mzazi au mlezi yeyote anayetaka kukagua, wakati wa saa za kazi za ofisi ya shule kabla na wakati wa mwaka wa shule kwa kuweka miadi. Ili ukague nyenzo, tafadhali wasiliana na mwalimu wa afya na siha wa mtoto wako.

Wazazi wanaweza kuchagua kutojumuisha watoto wao kwenye mafunzo ya maisha ya familia. ***Ikiwa hungependa mtoto wako ashiriki kwenye mafunzo ya Maisha ya Familia, tafadhali tuma barua kwa mwalimu wa mtoto wako kabla mafunzo hayajaanza (angalia tarehe ya kuanza kwa mafunzo hapo chini).*** Tafadhali weka jina kamili la mtoto wako, gredi na jina la shule kwenye barua hiyo. Kwa watoto ambao hawajumuishwi, mwalimu atapanga masomo mbadala ya kuchukua nafasi ya masomo ya Elimu ya Maisha ya Familia. Ikiwa ungependa mtoto wako apokee mafunzo ya Elimu ya Maisha ya Familia, huhitaji kuchukua hatua yoyote.

Ikiwa ungependa kukagua viwango vya mafunzo ya Elimu ya Maisha ya Familia, nakala hiyo ya viwango vya mafunzo inapatikana: [HAPA](#). Ikiwa una maswali kuhusu kipengele chochote cha Mpango wetu wa Maisha ya Familia katika Hampton City Schools, tafadhali usisite kuwasiliana na ofisi ya Elimu ya Afya na Siha.

Mada Zinazofundishwa katika Elimu ya Maisha ya Familia kwa kila gredi.

Gredi ya 4	FLE 4.1 Uwezo wa kubaini viungo vya uzazi vya binadamu FLE 4.2 Kubaini mabadiliko ya mwili yanayoanza kutokea wakati wa kubalehe FLE 4.4 Kubaini hisia za msingi za binadamu na njia bora za kukabiliana nazo
Gredi ya 5	FLE 5.1 Kubaini muundo na utendakazi wa mfumo wa endokrini FLE 5.2 Kubaini viungo vya uzazi vya binadamu kwa uhusiano na anatomia ya jumla FLE 5.4 Kutambua uhusiano kati ya mabadiliko ya mwili yanayotokea wakati wa kubalehe na ukuaji unaotokea kwenye viungo vya uzazi FLE 5.7 Kufafanua athari za usafi binafsi kwenye dhana ya mtu kujihusu FLE 5.9 Kukuza uelewa wa kina kuhusu kanuni, majukumu na wajibu wa wanafamilia.

Mafunzo ya Maisha ya Familia yatafanyika _____.